Wallahi – akipenda Mwenyezi Mungu - sitokula kiapo cha jambo fulani isipokuwa ninapoona kilichobora zaidi basi huwa ninatoa kafara ya kiapo changu kisha ninafanya lililo bora zaidi.”

Kutoka kwa Abuu Musa Al-Ash'ary radhi za Allah ziwe juu yake amesema: Nilikuja kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu rehema na amani ziwe juu yake nikiwa na kundi la Ash’ari ili kumuomba atuchukue, akasema: “Wallahi sitokuwa na chochote cha kukubebeni ” Kisha tukakaa muda kidogo aliopenda Mwenyezi Mungu tukae, tukaletewa ngamia, akaamrisha tupewe wanyama watatu kwa ajili yetu, tulipoondoka wakasema baadhi yetu kuwaambia wengine: Mwenyezi Mungu hatotubariki, tumemuendea Mtume rehema na amani ziwe juu yake tukamuomba atubebe katika vipando lakini akaapa kuwa hatotubeba, kisha akatubeba, akasema Abuu Musa: Basi tukaja kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake tukamueleza hilo, akasema: “Si mimi niliyekubebeni, bali Mwenyezi Mungu ndiye aliyekubebeni Wallahi – akipenda Mwenyezi Mungu - sitokula kiapo cha jambo fulani isipokuwa ninapoona kilichobora zaidi basi huwa ninatoa kafara ya kiapo changu kisha ninafanya lililo bora zaidi.”

[Sahihi] [Wamekubaliana Bukhari na Muslim juu ya usahihi wake]

Anasimulia Abuu Musa Al-Ash’ari radhi za Allah ziwe juu yake kuwa, alikuja kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu rehema na amani ziwe juu yake akiwa na kundi la kabila lake, na makusudio yao yalikuwa kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, ili awape ngamia wapande, ili kuweza kushiriki katika jihadi, aliapa rehema na amani ziwe juu yake kuwa hatowabeba, na hakuwa hana chochote cha kuwabeba, basi wakarudi na kukaa kwa muda, kisha wakaletewa ngamia watatu kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake akawatumia wale mabwana, baadhi yao wakaambiana: Mwenyezi Mungu asitubariki kwa ngamia hawa; Kwa sababu Mtume rehema na amani ziwe juu yake aliapa kutotubeba, basi wakamjia na wakamuuliza, akasema rehema na amani ziwe juu yake: Aliyekubebeni ni Mwenyezi Mungu Mtukufu; Kwa sababu yeye ndiye aliyetoa ufanikishaji na akaruzuku, lakini mimi ni sababu ya haya kutokea kupitia mikono yangu, kisha akasema rehema na amani ziwe juu yake: Wallahi, akipenda Mwenyezi Mungu, sitaapa kufanya au kuacha chochote, na nikaona kuwa kisichokuwa kiapo hicho ni heri na bora zaidi, isipokuwa nitafanya lililo bora zaidi, na kuyaacha niliyoapa, na ninalipa kafara ya kiapo changu.